**OR - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO**
**SHULE YA SEKONDARI MZALENDO**
**S.L.P 101 TUKUYU**
E-mail; mzalendosecondary328@gmail.com
Phone; 0765298422/0719562290 MKUU WA SHULE
MAKAMU MKUU WA SHULE: 0763673085 /0719 000 438

**YAH; MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MZALENDO MWAKA 2021.**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Mzalendo kidato cha ……… Shule itafunguliwa tarehe 11.12.2020. Ni mahali pazuri kwa ajili ya mafanikio ya kitaaluma.

**FIKA NA MAHITAJI YAFUATAYO**

1. **Sare ya shule**

   ***a) Wasichana***

   i) Sketi 2, 1 dark blue na 1 damu ya mzee ziwe ndefu pamoja na scaff/ necktie mbili kufuatana na rangi ya sketi (vitambaa vimeambatanishwa)
   ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi
   iii) Soksi nyeupe jozi mbili, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi na viwe vya kufunga kwa Kamba
   iv) Sweta mbili za kijani
   v) Tracksuit rangi ya light blue pamoja na raba kwa ajili ya michezo

   ***b) Wavulana***

   i) Suruali 2, 1 dark blue na 1 damu ya mzee zenye mkunjo chini na malinda mawili mbele pamoja na tai 2 kufuatana na rangi ya vitambaa vya suruali (vitambaa vimeambatanishwa)
   ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi
   iii) Soksi nyeusi jozi mbili, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi na viwe vya kufunga kwa kamba
   iv) Sweta mbili kijani
   v) Tracksuit rangi ya light blue pamoja na raba kwa ajili ya michezo

2. **Vifaa vya darasani**

   i) Daftari tisa counterbooks, mkebe 1(mathematical set) biki na penseli
   ii) Faili moja kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za mitihani
   iii) Bunda moja la karatasi
   iv) Kamusi yenye fasili ya kiingereza na Kiswahili

v) Picha 2 za passportsize ya rangi kwa ajili ya kubandika kwenye faili na darasani

**3. Mahitaji mengineyo muhimu kwa wanafunzi wa kutwa**

i. Vifaa vya usafi jembe lenye mpini moja na mfagio mmoja wa chelewa
ii. Mahindi yaliyokobolewa debe moja na nusu, maharage bipii nane(kimbo /mpishi nane) na chumvi pakiti 4 kwa mwaka
iii. Shilingi elfu tano kwa ajili ya malipo ya mpishi na mahitaji ya chumvi na mafuta kwa mwaka
iv. Sahani na kijiko kwa ajili ya chakula

**KARIBU MZALENDO SEKONDARI**

Eddy Odward Mwasomola
**MKUU WA SHULE**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## SHERIA ZINAZOTUONGOZA SHULE YA SEKONDARI MZALENDO

1. Ukiwa ni mwanafunzi wa shule hii, unatakiwa kutumia akili yako vizuri kwa mambo yote uyatendayo.

**2. KUSOMA NA MAHUDHURIO**

a) madhumuni makuu ya kuja kwako hapa shuleni ni kupata Elimu,hivyo ni jukumu la kila mwanafunzi kusoma kwa bidii kwa manufaa yake mwenyewe na familia yake, shule na Taifa pia.

b) Kuhudhuria darasani ni lazima, kila mwanafuzl awepo darasani kwa utuiivu,amani na adabu muda wote wa darasani

c) mwanafunzi atakayeshindwa kuhudhuria darasani kwa siku 2l mfululizo pasipo sababu ,zinazoeleweka na uongozi wa shule atakuwa amejikosesha na kujifuta shule mwenyewe.

d) kwa muda wote utakapokuwapo hapa shuleni lugha pekee inayotumika ni kiingereza na Kiswahili kwa mawasiliano yote, lugha za asili haziruhusiwi.

**3. MIPAKA YA SHULE**

a) Mwanafunzi anatakiwa muda wote awepo ndani ya mipaka ya shule pindi anapokuwapo shuleni, ni marufuku kwa mwanafunzi kuwepo nje ya mipaka ya shule kwa muda na masaa yote ya muda wa shule pasipo kibali maalumu, hii ni pamoja na kutembelea katika nyumba na makazi ya walimu.

b) Pia ni marufuku kwa mwanafunzi kuonekana katika nyumba za wageni, vilabu vya pombe na kwenye magenge ya vijiwe vya wavutaji na wahuni.

c) Mwanafunzi anapokuwa nyumbani hatarajiwi kuzurura hovyo zaidi ya saa 1:00 usiku ni makosa kwa sheria ya shule.

**4. SARE YA SHULE**

a) Kila mwanafunzi atatakiwa kuwa katika vazi rasmi la shule muda na saa za shule maeneo ya shuleni, njiani anapokuja shule na anaporudi nyumbani na katika mikusanyiko rasmi ya shule nje ya shule na ni marufuku mwanafunzi kuvaa sare za shule mitaani siku ambazo sio za shule bila kibali na ruhusa kutoka shule, marufuku hii inaenda sambamba na mapambo na urembo wowote ni marufuku.

**5. HESHIMA NA KUJIHESHIMU**

a) Hii ndio nguzo yetu kuu ya nidhamu ya shule kwa kuheshimu wakubwa na wenzake, kila mwanafunzi inampasa kuwa na mwenendo bora njiani kwa jamii, walimu na wafanyakazi wasio

walimu kwa kuwaheshimu na kuonyesha nidhamu bora wakati wote.

b) kuheshimu bendera ya TAIFA, wimbo wa TAIFA, fedha ya nchi, uongozi wa nchi na wimbo wa shule.

c) Ni marufuku na huruhusiwi kutumia lugha chafu kwa mtu yeyote na katika mazingira yoyote nani na nje ya shule.

**6. USAFI**

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia usafi wa mwili kuanzia kucha mpaka nywele, mavazi na mazingira.

b) Ni marufuku kuwa na kucha ndefu, kunyoa mitindo isiyostahili, kupaka rangi/dawa nywele na mambo yote yanayokuwa kinyume na mazingira ya shule.

**7. UTII**

a) Kila mwanafunzi anapaswa kutii kengele mara moja kwa kukimbia.

b) Kila mwanafunzi anapaswa kutii mara moja wito wa mwalimu/watumishi/viraja mara anapitwa kwa kukimbia.

**8. UTUNZAJI WA MALI ZA SHULE**

**Mali ya Shule/Jumuiya**

a) Ni jukumu la kila mwanafunzi kutunza au kutumia kwa uangalifu mali yoyote ya shule kama vitau, viti, meza, vifaa vya maabara na majengo.
b) Kuweka maandishi ya aina yoyote ile kwenye kuta, viti, meza na mahali popote pasipostahili ni uharibifu wa mali ya shule. Pia usitumie ubao wa shule bila idhini ya mwalimu.
c) Kitendo chochote kitakachosababisha uharibifu au upotevu wa mali ya shule kwa uzembe kitapelekea kufukuzwa shule ama kufidia uharibifu au upotevu huo.

**Mali binafsi:**

a) Mali yoyote ya binafsi itunzwe kwa uangalifu.
b) Mwanafunzi anashauriwa kuepukana na utunzaji wa fedha kwa mwanafunzi mwenzake.
c) Wizi na matatizo mengine yanayoambatana na upotevu wa mali sharti uripotiwe kwa kiongozi anayehusika mara moja.

**9. UHUSIANO NA JAMII**

a) Hakuna mwanafunzi yeyote anayeruhusiwa kutoa maelezo yanyohusiana na shule hii kwa mtu wa nje bila kupata idhini ya mkuu wa shule.
b) Mwanafunzi haruhusiwi kujiingiza kwenye mikataba au mikopo ya aina yoyote ile na watu wa nje bila idhini ya mkuu wa shule.
c) Mwanafunzi anapotembelea mahali popote pale, hana budi kuheshimu, kutii na kufuata sharia za mahali pale.

d) Mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha na biashara ama michezo inayohusiana na fedha muda wote awapo shuleni.

## 10. MAMBO YANAYOWEZA KUMFANYA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE

a) Wizi
b) Uasherati, ubakaji na ushoga
c) Ulevi wa pombe aina zote
d) Matumizi ya madawa ya kulevya kama bangi, cocaine, mandraz n.k
e) Makosa ya jinai
f) Kupiga au kupigana
g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
h) Kudharau bendera ya Taifa au wimbo wa Taifa
i) Kuoa au kuolewa
j) Kusababisha mimba ndani na nje ya shule
k) Kupata mimba au Kutoa mimba
l) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
m) Kukataa adhabu kwa makusudi

## 11. UTII WA SHERIA ZINGINE

a) Kila mwanafunzi anapaswa kufuata ratiba ya kila siku ya shule
b) Kila mwanafunzi anapaswa kutii na ufuata sharia za Nchi pamoja na sharia ndogo zilizowekwa na mamlaka mbalimbali.
c) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu katika maeneo ya shule.

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI KIDATO CHA KWANZA 2021**

1. Jina kamili ……………………………..…………………………………..……………….
2. Mahali alipozaliwa ………………………………………..…………………………….
3. Tarehe ya kuzaliwa ………………………….………………………………………….
4. Jina la baba ………………………..hai/marehemu……..………………… kama ni mzima, anafanya kazi gani? ………………………… namba ya simu ………………..…………..
5. Jina la mama …………………………… hai/marahemu………………kama ni mzima, anafanya kazi gani? …………………… namba ya simu…………………………………..
6. Je mama na baba wanaishi pamoja? ……………………… kama hapana; Je, wewe unaishi na nani? ………………………………………….
7. Kama yatima jina la mlezi………………………kazi anayofanya…………………… namba ya simu……………………uhusiano na mlezi……………….…………………….
8. Anwani ya mzazi /mlezi ……………………………………………………………….
9. Shule ya msingi uliyotoka ……………………………………………………
10. Dhehebu/ Dini ……………………………………………………………
11. Nathibitisha kuwa habari nilizotoa ni za kweli na sahihi.

Saini ya mwanafunzi ……………………………. Tarehe…………………………………….

Saini ya Mzazi/Mlezi ……………………………. Tarehe …………………………………..

*Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule unaporipoti shuleni.*

## MEDICAL CERTIFICATE FORM

STUDENT NAME……………………………………………………………………………

To be completed by a Government Medical Officer or a doctor from a recognized health institution in respect of form one entrant. Please examine the above as to her/his physical and mental fitness as a student at this school.

The examination should have to involve the following categories

i. Vision with glasses right …………………………… left……………………
ii. Blood pressure ……………………………………………………………
iii. Hemoglobin ………………………………………………………………
iv. F. V. Bleeding ……………………………………………………………
v. Urine for sugar. …………………………………………………………
vi. Stool for routine examination ………………………………………………
vii. Venereal diseases …………………………………………………………
viii. Neurosis ……………………………………………………………………
ix. T. B. Test …………………………………………………………………

10. Any abnormality

a) Heart ……………………………………………………………………
b) Lung ……………………………………………………………………
c) Spleen ……………………………………………………………………
d) Chest ……………………………………………………………………

11. Is there any serious disease e.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma,

Diabetes ……………………………………………………………………

Doctor's name…………………………………………………………

Signature and official stamp

…………………………………

Date …………………………………